TANGAZO LA SERIKALI NA. 234 la tarehe 24/3/2023

SHERIA YA MIPANGO MIJI
(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa Chini ya Kifungu cha 8(1) na 23(1))*

AMRI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWA ENEO LA TINDE YA MWAKA, 2023.

Jina:

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kurasimisha Makazi yasiyopangwa Eneo la Tinde ya mwaka, 2023

Utangazaji wa Eneo la Upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji (mpango wa urasimishaji) kwa madhumuni ya Sheria ya Mipango Miji.

Mpango katika eneo la kwenye Jedwali

3. Mipango ya jumla na kina kwa eneo lililoainishwa katika Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipango Miji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la urasimishaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:-

"Unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba A yenye majira - nukta 519424.704MS, 9573486.621KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Mashariki katika uelekeo wa KZ69º 40'36.71''MS kwa umbali wa kilomita 2.808 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba B yenye majira - nukta 522058.228MS, 9574462.000KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Mashariki katika uelekeo wa KZ84º44'12.40''MS kwa umbali wa kilomita 2.343 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba C yenye majira - nukta 524392.332MS, 9574677.017KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini katika uelekeo wa KS12º31'43.69''MG kwa umbali wa kilomita 0.452 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba D yenye majira - nukta 524294.123MS, 9574235.079KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini katika uelekeo wa KS25º09'33.49''MS kwa umbali wa kilomita 0.895 kwa kukatiza barabara ya Shinyanga - Tabora hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba E yenye majira - nukta 524674.681MS, 9573424.858KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini katika uelekeo wa KS06º31'11.28''MS kwa umbali wa kilomita 0.432 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba F yenye majira - nukta 524723.786MS, 9572995.195KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Magharibi katika uelekeo wa KS69º25'47.24''MG kwa umbali wa kilomita 1.305 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba G yenye majira - nukta 523033.607MS, 9572341.526KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Mashariki katika uelekeo wa KS39º27'22.69''MS kwa umbali wa kilomita 0.942 hadi kwenye alama ya mpaka ya upiamji namba H yenye majira - nukta 523632.490MS, 9571613.893KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini katika uelekeo wa KS12º21'36.65''MG kwa umbali wa kilomita 1.294 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba I yenye majira - nukta 523355.482MS, 9570349.801KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Mashariki katika uelekeo wa KZ77º09'19.47''MG kwa umbali wa kilomita 1.842 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba J yenye majira - nukta 487343.805MS, 9623343.759KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini katika uelekeo wa KS20º12'23.11''MG kwa umbali wa kilomita 1.496 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba K yenye majira - nukta 521041.883MS, 9569354.915KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi katika uelekeo wa KZ64º07'52.13''MG kwa umbali wa kilomita 2.441 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba L yenye majira - nukta 518845.329MS, 9570420.029KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini katika uelekeo wa KZ10º41'55.88''MG kwa umbali wa kilomita 3.120 ukikatiza barabara ya Shinyanga - Kahama hadi ulipoanzia."

Dodoma,
6 Februari, 2023

BANGELINE S. MABULA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*